



## **TAARIFA KWA UMMA**

### **WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT MUJIBU WA SHERIA MWAKA 2024**

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), linawaita Vijana waliohitimu elimu ya sekondari kidato cha sita kwa mwaka 2024 kutoka Shule zote za Tanzania Bara kuhudhuria Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2024.

Sanjari na wito huo, JKT limewapangia makambi watakayo kwenda kupatiwa Mafunzo na wanatakiwa kuripoti makambini kuanzia tarehe 01 Juni hadi 07 Juni 2024.

Vijana hao wamepangwa katika Kambi za JKT Rwanakoma - Mara, JKT Msange - Tabora, JKT Ruvu - Pwani, JKT Mpwapwa, Makutupora JKT - Dodoma, JKT Mafinga - Iringa, JKT Mlale - Ruvuma, JKT Mgambo na JKT Maramba -Tanga, JKT Makuyuni - Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa na JKT Mtabila - Kigoma, JKT Itaka - Songwe, JKT Luwa na JKT Milundikwa - Rukwa, JKT Nachingwea – Lindi, JKT Kibiti- Pwani na Oljoro JKT- Arusha.


Aidha JKT linawataka vijana hao kuripoti wakiwa na vifaa vifuatavyo.

1. Bukta ya rangi ya 'Dark Blue' yenyе mpira kiunoni, iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini, isiyo na zipu.
2. T-shirt ya rangi ya kijani (Green Vest)
3. Raba za michezo zenyе rangi ya kijani au blue.
4. Shuka mbili za kulalia zenyе rangi ya blue bahari.
5. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
6. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenyе baridi.
7. Track suit ya rangi ya kijani au blue.
8. Nyaraka zote zinazohitajika katika Udhili wa Kujiunga na Elimu ya Juu, zikiwemo cheti vya Kuzaliwa, Vyeti vya Kuhitimu kidato cha Nne nk.
9. Nauli ya kwenda makambini na kurudi nyumbani.

Orodha kamili ya majina ya vijana hao, Makambi ya JKT waliyopangiwa na maeneo Makambi hayo yalipo na vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, Inapatikana katika tovuti ya JKT ambayo ni [www.jkt.go.tz](http://www.jkt.go.tz)

Aidha, majina hayo pia yanapatikana kupitia simu ya mkononi, kwa mtumiaji kupiga **USSD CODE \*152\*00#, kisha atachagua No 8 (Elimu) ikifuatiwa na No 5 (JKT)**, ambapo mtumiaji ataingiza namba ya shule aliyosoma ikifuatiwa na majina yake matatu kisha mtumiaji ataoneshwa kambi alilopangiwa na mahali ilipo. Huduma hii inapatakanwa kwa watumiaji wa mitandao yote ya simu nchini.

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, anawakaribisha vijana waliohitimu kidato cha sita mwaka 2024 kuungana na Vijana wenzao ili kujengewa Uzalendo, Umoja wa Kitaifa, kufundishwa stadi za kazi, Stadi za Maisha na Utayari wa Kulijenga na Kulitumikia Taifa lao.

  
BngGen

**Imetolewa na:  
Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,  
Makao Makuu ya JKT,  
Tarehe 24 May 2024.**